**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu.**

**Mkuu wa Shule 0623673740**

**Makamu Mkuu wa Shule 0620151103**
**Matron/ Patron 0768039829/0758083877**

**Shule ya Sekondari Kasangezi**

**S.L.P.315**

**Tarehe ……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI HALMASHAURI YA KASULU MKOA KIGOMA MWAKA……………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka………. na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ya Sekondari KASANGEZI ipo umbali wa Kilometa 27 Kusini mwa Mji wa Kasulu, Usafiri wa basi/daladala kutoka mjini Kasulu unapatikana katika kituo cha mabasi/daladala makabulini/stendi mpya kwa nauli ni Shilingi elfu tatu (3000/=) tu.

**Mhula wa Masomo unaanza tarehe ……..…. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……….**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili (2) za dark blue(kitambaa kizito) na shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi kwa Wasichana, na suruali mbili (02) za dark blue (kitambaa kizito) na shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi kwa Wavulana, mshono wa kawaida kwa wavulana, suruali isiwe ya kubana(modo) na iwe na mkunjo wa chini (turn up), kwa wasichana sketi inatakiwa ifike kwenye jicho la mguu(juu kidogo ya unyayo), mshono ni linda boksi.**Siyo jukumu la shule** kushona sare za wanafunzi **ILA** wazazi watakaopenda kushona sare hizo shuleni wataelekezwa sehemu ya kupata sare hizo kwa kwa gharama zifuatazo:(sketi 2@16000= Tshs.32000, Suruali 2@14000 = Tshs 28000/=).

ii. Rangi ya Hijab (kijuba) kwa anaye hitaji ifanane na kitambaa cha shati ya shule na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iii. Sare ya Michezo kwa shule hii, ni jezi za blue ya chelsea ziwe mbili (T-shirt za bluu mikono mifupi na truck suit ya bluu yenye mistari myeupe pembeni kwa wasichana na kwa wavulana. Ziwe kuanzia pair mbili (2)).

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/khaki za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta la rangi ya dark bluu, mikono mirefu isiwe na mistari wala maandishi yoyote.

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) kitambaa kizito rangi ya ‘damu ya mzee’. Wanafunzi waje na nguo hizo, **Siyo jukumu la shule** kushona sare za wanafunzi **ILA** kwa wale wazazi/walezi watakaopenda wanafunzi washonewe karibu na shule wataelekezwa mahali pa kuzipata kwa gharama zifuatazo,Kwa wasichana ni gauni mbili (02) za rangi ya damu ya mzee(kitambaa kizito), zinapatikana kwa gharama ya 2@20000= Tshs.40,000/= Pia kwa wavulana ni suruali mbili (2) rangi ya damu ya mzee(kitambaa kizito) zinapatikana kwa gharama ya 1@14000 = Tshs.28,000/=.

ix. Wanafunzi waje na T-SHIRT za rangi ya ‘**bluu bahari’** zenye kora zisizo na maandishi ya aina yoyote,na kwa wale wazazi/walezi **watakaopenda**, T-shirt hizo zinapatikana shuleni kwa gharama ya **TZS: 12000 TU**.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari tisa (06) quire 3.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi tatu (3) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro size 2.5 x 6.
vii. Mashuka Jozi 2 pink kwa wasichana, blanket 1, foronya ya godoro 1 yenye rangi ya shuka, chandarua 1.
viii. Mashuka jozi 2 bluu kwa wavulana na foronya 1 yenye rangi ya shuka, blanket 1, na chandarua rangi ya bluu .
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xii. **Kwanja 1**(kwa wanafunzi wa tahasusi za HGL,HGK,EGM, na HKL), **Jembe 1**(Kwa wanafunzi wa PCM,PCB na CBG), Mopa 2, Mifagio 2, ya ndani na nje.

**Kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi yani PCM,PCB na CBG kila mwanafunzi anapswa kununua vitabu vifuatavyo.**

1. **Chemistry**
   i. Modern ABC class XI and Class XII
   ii. Advanced level chemistry topical review Book 1&2 by Mr. A.Mandia(new Sylubus
   iii. Advanced level chemistry practical by Mr. A.Mandia (new Sylubus 2024)
   iv. Organic chemistry for advanced level by Mr.A.Mandia (new sylubus 2024)
   v. Solution manual for advanced level chemistry books by Mr.A.Mandia (new sylubus 2024)
2. **Biology**
   i. Biology for Advanced level topical review Book 1&2 by Mr. A.Mandia(new sylubus 2024)
   ii. Advanced level Biology practical by Mr. A.Mandia(new Sylubus 2024)
   iii. Solution manual for advanced level biology books by Mr.A.Mandia (new sylubus 2024)

**3. physics**

i. Chand class XI and class XII

**4. advanced mathematics**

i. Pure mathematics 1&2 by Backhouse
ii. Advanced level pure mathematics by CJ Tranter
iii. Scientific calculator Fx-991
iv. **Chand class XI and XII**
v. **Competence Based Advanced mathematics for secondary schools form 5 & 6 by Mayombya P L.**
vi. Graph paper
vii. Mathematical set

**ENGLISH**

1. A BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN
2. A MAN OF THE PEOPLE BY CHINUA ACHEBE
3. HIS EXELLENCE THE HEAD OF STATE BY DANSAFO
4. THE WOUNDERFUL SUGEON BY CHARLES MLOKA
5. BETRAYAL IN THE CITY BY FRANCIS IMBUGA
6. AN ENERMY OF THE PEOPLE BY ERICK IBSEN
7. I WILL NARRY WHEN I WANT BY NGUGI WA THIONGO&NGUGI WAMII
8. SELECTED POEMS BY TIE
9. THE OXFORD ADVANCED LEARNERS DICTIONARY
10. ADVANCED LEVEL ENGLISH A PRACTICAL APROACH BY NICHOLOUS ACHERY

**GEOGRAPHY**

1. GEOGRAPHY AN INTERGRATED APPROACH BY DAVID WAUGH
2. HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY BY GOH CHONG LEONG,GILLIAN C MORGAN
3. PRACTICAL GEOGRAPHYBY PITCHED
4. ELEMENTARY PHYSICAL GEOGRAPHY BY AHMED LUBWAMA

**KISWAHILI**

1. KISWAHILI-1 (KIDATO CHA 5&6 )BY KILANGI ENOCK LUCA
2. CHUNGU TAMU MWANDISHI T.A MVUNGI
3. FUNGATE YA UHURU MWANDISHI MOHAMED SEIF KHATIB
4. KIMBUNGA MWANDISHI HAJI G HAJI

**HISTORY**

ESSENTIAL ISSUE IN HISTORY PAPER (1&2)BY YASIN

Tanbihi:

Vitabu vya Mr Mandia vinapatikana sehemu tofauti tofauti kwa Dar es Salaam vinaptikana Msimbazi centre office number 22,kwa wale wanaotokea mkoa wa Arusha na kilimanjaro vinapatikana shule ya msingi makumbusho iliyopo kaloleni kwa dodoma vinapatikana Co-brothers phamacy mkabala na Dodoma general hospital

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: MICHANGO TAJWA HAPO JUU IWEKWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE.**
**JINA LA AKAUNTI: KASANGEZI SECONDARY SCHOOL CAPITATION.**
**AKAUNTI NAMBA: 51401200147**
**BANK: NATIONAL MICROFINANCE BANK (NMB)**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,

inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule Charles Lugenda**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0623673740.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0620151103/0752969602**
- **Mwandamizi Taaluma 0759390874**
- **Mwandamizi Malezi 062788802**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

A.Maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi

1. Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………………………
2. Mahali anapoishi Kijiji/mtaa…………………………….Mkoa……………………wilaya……………
3. Tarehe ya kuzaliwa…………………Kijijialichozaliwa…………………..kabila……………..
4. Shule ya sekondari(''O''level)aliyosomea…………………………………………………

Habari za wazazi/walezi

1. Jina kamili la baba/mlezi ………………………………………………………………………………
2. Jina kamili la mama/mlezi ……………………………..……………………………………
3. Kazi ya baba/mlezi…………………………………….......……………………………… Kaz ya mama/mlezi………………………………………………………………………
4. Je baba yupo hai. Ndiyo/hapana.
5. Je mama yupo hai .ndiyo/hapana. Kukitoke adharura ndugu wengine wanaoweza kujulishwani:-

1. Jina kamili………………………………………….uhusiano uliopo…........................namba ya simu…..……………...
2. Jina kamili………………………………………Uhusiano uliopo…...........................namba ya simu………………….. Mimi.................................................................niliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari kasangezi kidato chatano(5)mwaka2025.

Mimi..................................................................Nathibitisha kuwa taarifa hizo ni sahihi na zakweli

Jina kamili la mzazi/mlezi………………………………Saini………………………………Simu…………

B.Mkataba wa kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai.

1. Naahidi kutii na kutekeleza masharti na maelekezo mbalimbali ya shule chini ya uongozi wa shule.Sitashiriki katika migomo,fujo na makosa yoyote ya jinai
2. Kama mwanafunzi na ahidi kuwa mtiifu na mnyenyekevu mahali popote kwa kuzingatia kanuni,taratibu na sharia za shule hii
3. Endapo ni takiuka kanuni,taratibu na sharia za shule hii na stahilikuadhibiwa kulingana na itakavyoelekezwa na kuamriwa na mwalimu,mkuu wa shule na bodi ya shule kwa ajili ya kurekebisha mwenendo wangu,kuleta heshima ya shule,kuletaamaninautulivu shule nina kuendeleza malezi bora kwa vijana wa Tanzania
4. Nathibitisha kuwa nimesoma kwa makini na matamko haya na yatakuwa kwa ajili yangu mwenyewe. Jina la mwanafunzi…………………Saini…………… tarehe………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU**
**SHULE YA SEKONDARI KASANGEZI.**

Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

1Mimi ........................................................................................................ mzazi/mlezi wa mwanafunzi.........................................................................aliyechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari kasangezi mwaka 2024.

2. Nakubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule kwani natambua kuwa malezi bora ya motto ni matunda kati ya walimu na wazazi/walezi

3. Aidha natambua kuwa nidhamu ina mchango mkubwa katika maendeleo mazuri ya kitaaluma ya mwanafunzi.

4. Aidha natambua kuwa nidhamu ina mchango mkubwa katika maendeleo mazuri ya kitaaluma ya mwanafunzi. Jina kamili la mzazi/mlezi…………………………………………………

Namba ya simu………………………………………………

Saini…………………………………………

Tarehe……………………………………………………………

## (REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)

## KASANGEZI SECONDARY SCHOOL
## MEDICAL EXAMINATION FORM

Student'sfull name…………………………………………………………………..
Age…………………(years)……………………………………………………………..
Sex…………………………………
Stool examination…………………………………………………………...
Urinalysis………………………………………………………………………………………
…………………………………………
Blood count.........................................................................................................................
……………………………………..………………………………….................................
Syphilis est.……………………………………………………………………………………
………………………………................................................................................................
T.BTest…………………………………………………………………………………………
Eyetest.…………………………………………………………………………..……
………………………………..................................................................................................
Spleen……………………………………………………………………………………………
..…………………………………
Pregnancy:............................................................................................................................
Chest.......:................................................................................................................................
Hearring:...................................................................................................................................
Heart..........................................................................................................................................
Stomach ulcers.........................................................................................................................
Any physical defects,impairements,chronic infections or family diseases if any....................................
……………………………………………………………………………………………......
…………………………………………………

Icertify that I have examined above student and recommended that he/she is fit/unfit to pursue further education.

Name of Medical Officer………………………………..Designation…………………………

Station………………………..Signature and Stamp……………………..Date…………………